**BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE**
AN AGENCY OF THE BAPTIST MISSION OF EAST AFRICA
TELEPHONE 58744 · P. O. BOX 30370 · NAIROBI, KENYA

# IWE NURU



## MWANAMKE MPYA KATIKA KRISTO

# IWE NURU

## APRILI, MEI, JUNI
## 1982

## Y A L I Y O M O

**APRILI:** **MWANAMKE MPYA:**
Bi. Betty Ann Whitson

1. Ya Kale Yawekwe Mbali
2. Mwanamke Mpya Katika Kristo
3. Mwanamke Mpya Nyumbani
4. Mwanamke Mpya Katika Jamii na Kanisani

**MEI:** **UPEO WA MAISHA YA KIROHO**
Bi. Betty Ann Whitson

1. Katika Kuhudhuria Kanisani
2. Katika Maombi
3. Katika Mafunzo ya Biblia
4. Katika Uwakili Binafsi

**JUNI:** **USHUHUDA WA MAISHA YA KILA SIKU**
Bi. Helen Gilmore

1. Ushuhuda Katika Jamii na Nyumbani
2. Ushuhuda Katika Kuwafundisha Watoto
3. Ushuhuda Binafsi
4. Rwanda, ............. Bi. Jane Martin

**MISAADA MAALUM:** **KAZI YA KUSHONA**
Grace Wairimu

©
Copyright, 1982
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and printed by
Baptist Publications House
Box 30370, Likoni Road, Nairobi

kanisa moja la pekee ililoko Kigali. Kanisa hilo ni changa au mpya.

**Sehemu ya Nne:** Mnyarwanda Mkristo Kiongozi

Bwana Josia, ambaye ni Mnyarwanda, aliendа katika nchi ya Uganda kutafuta kazi akiwa kijana. Alipokuwa kule alimpokea Yesu kama Mwokozi wake. Aliingia katika Chuo cha Kujifunza Biblia na halafu akaanza kuhubiri katika nchi ya Uganda. Katika mwaka wa 1977, makanisa yalipofungwa katika nchi ya Uganda, Josia alirudi katika nchi yake aliyozaliwa ya Rwanda. Alikaa katika eneo la kwao na kila mahali alipoenda aliongea na watu habari za Mwokozi wake. Alianza kuhubiri chini ya mti na watu wengi wakapata kusikia Habari Njema. Kanisa lilianzishwa katika eneo hili, lililokuwa likikutana chini ya mti. Baadaye aliombwa kwenda kwa kanisa la Kibatisti lililokuwa na shida. Yeye pamoja na mke na watoto wao walihamia sehemu hiyo ya eneo hilo mpya. Jumapili ya kwanza kulikuwa na watu kumi, Jumapili iliyofuata kulikuwa na watu arobaini. Kwa hiyo kazi iliendelea kukua. Sasa kanisa lina uhuisho tena. Josia hawezi kuacha kuhubiri habari za pendo lake Mungu na juu ya kipawa chake cha wokovu.

**Kiongozi:**

Jamaa wengi huwa na watu wengi walio na mashamba madogo. Wakati ambao hamna mvua ya kutosha, huwa na ukosefu wa chakula. Watu wengi bado hawajasikia Habari Njema za Yesu Kristo. Watu wengi wanalijua Jina Lake, lakini hawajamjua kama ni Mwokozi wao. Sehemu nyingi za nchi hazijafikiwa kwa kupelekewa Kristo.

**Maombi:**

Uombe ili Mungu awaite wavulana na wasichana kuwa viongozi. Uombe kwamba roho wa ufufuo amiminike ndani ya makanisa yetu.





Mpango wa Kwanza

## YA KALE YAWEKWE MBALI

**Maandiko Matakatifu:** 2 Wakorintho 5:14-20

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya.*
*2 Wakorintho 5:17*

**(Jambo Muhimu:** Kwa ajili ya mpango wa mwezi huu andika kifungu cha 2 Wakorintho 5:17 juu ya ubao au kwenye karatasi kubwa.)

**Utangulizi:**

Sisi tulio Wakristo tunayo maisha mapya katika Kristo. Kama tulivyosoma katika Wakorintho, ni lazima tuache utu wetu wa kale na kuwa kama viumbe vipya. Kazi hii ni ngumu na Wakristo wapya wote hawabadilishi njia zao mara moja. Mara nyingi ni wazito sana kuona kwamba ni lazima wamwache Kristo aonekane katika yote wafanyayo. Pengine mipango hii itakusaidia.

Tutaangalia maisha ya wanawake wawili ambao wanaishi kama unavyoishi. Wote wawili wamekiri imani katika Kristo. Tutawaita Elizabeti na Veronika. Wanaweza kuwa mfano wa mmoja wenu.

**Sehemu ya Kwanza:**

Elizabeti alipotembea njiani kuelekea nyumbani kwake, alionekana mwenye furaha sana. Hakutaka kungoja kumwambia mumewe Hamisi kile kilichofanyika asubuhi hiyo. Ndani alijiona kuwa safi na tofauti kwa vile sasa alimjua Yesu kama Mwokozi wake.

Mwokozi alikuwa ameishakuja kukaa katika moyo wake, na kwa hivyo ni lazima aishirikishe furaha hii kwa jamaa yake. Hakuna mtu ye yote kwao aliyepata kuwa Mkristo. Walikuwa wangali wakifuata njia za zamani za kabila lao.

Veronika, rafiki ya Elizabeti, aliishi karibu na mpaka wa mji. Alikuwa akienda nyumbani kutoka katika ibada ya asubuhi akijiona mwenye furaha rohoni mwake. Vile vile mwishoni mwa ibada alikuwa amesema ya kuwa atamwamini Yesu na atamfuata Yeye, lakini kulikuwa na wasiwasi rohoni mwake. Alikuwa na wasiwasi ya kile ambacho jamaa yake wangesema. Mumewe, Edward, angekasirishwa naye kwa sababu alikuwa ametoka shambani mapema sana siku ile ili aende kanisani. Mumewe alikuwa na kazi nzuri kama karani mjini na ilikuwa wajibu wa mkewe kukaa shambani na kufanya kazi humo. Alikata shauri kwamba hatamwambia mtu ye yote sasa juu ya kuwa Mkristo. Aliliweka jambo hilo kama siri.

**Sehemu ya Pili:**

Hamisi alimngojea mkewe kurudi akiwa na moyo wa hasira. Alitoka sokoni akiwa mwenye njaa sana. Chakula hakikuwa tayari. Alipomwona akija, alianza kupaza sauti kwa hasira. Elizabeti alisema alisikitika sana na alisema kuwa atampikia chakula upesi sana, lakini kitu maalum kilikuwa kimetendeka. Mashtaka mengi yalitoka kwa Hamisi, na kwa haraka alinyamaza. Tofauti ni nini? Kawaida ya Elizabeti ilikuwa kupiga mayowe wakati wa kumjibu mumewe, na kwa hiyo lazima kutokee magombano. Elizabeti alikuwa amebadilika kidogo. Ni nini kilichokuwa kimetukia?

Paulo, mtoto mvulana wa Veronika alikimbia kukutana na mamaye wakati alipomwona akitembea njiani iliyoelekea kwenye nyumba. Mtoto yule alimwambia mama yake kwamba kulikuwako na mtu ambaye alipenda kumwona mumewe. Alipofika, akamwona Abdullah, rafiki ya mumewe. Alikuwa





Watu hupanda viazi, maharagwe, mtama, kahawa, mihogo, viazi vya kizungu, njugu karanga na ndizi. Ndizi aina nyingi hukuzwa. Kwa bahati mbaya ndizi nyingi hutumiwa na watu katika kutengeneza pombe kali ya kienyeji. Mchele na chai hupandwa katika mashamba ya serikali.

**Sehemu ya Pili:** Dini Katika Nchi ya Rwanda

Nusu ya Idadi ya watu wote wa Rwanda ni wa dini ya Kirumi, kwa sababu ya kazi iliyofanywa na mapadre wamisheni waliowasili mapema kutoka nchi ya Ubeligiji na Ufaransa. Watu wachache ni wafuasi wa dini ya Kiislamu. Wale wengine ni wafuasi wa dini ya Kiprotestanti. Kutoka katika idadi ya watu wapatao milioni tano wa nchi hiyo ya Rwanda, watu wapatao 22,000 ndio Wabatisti. Kunalo hitaji kubwa la kuihubiri Injili ya Yesu Kristo. Watu wako tayari kuitikia mahubiri na mwito wa Neno. Wabatisti wamekuwa wakisaidia nchi ya Rwanda kwa zaidi ya miaka thelathini.

**Sehemu ya Tatu:** Wamisheni Katika Nchi ya Rwanda

Wamisheni waliotoka nchi ya Denmark na Sweden walikuwa wamefanya kazi kwa muda wa miaka mingi katika nchi ya Rwanda. Wengi wao waliondoka wakati wa mabadiliko ya serikali. Baada ya kujifunza lugha ya Kifaransa na lugha ya Kinyarwanda, jamaa mbili za wamisheni wa kutoka Amerika watakwenda kuanza kufanya kazi zao katika mkoa wa nchi hiyo uitwao Mukoma. Jamaa moja itasaidia makanisa katika uinjilisti na uwakili. Nayo jamaa ile nyingine itakuwa na kazi mbili maalum. Mwanamume ni Daktari wa mifugo na atawasaidia wenyeji kwa kusitawisha na kutibu mifugo yao. Atawafundisha kufuga sungura kwa sababu ya kupata chakula cha nyama. Pia kwa kuwa Daktari huyo ni mhubiri anapenda kuwaona watu wakimwendea Kristo. Mke wake amejifunza muziki. Madhumuni yake ni kwenda kila kanisa na kuwasaidia kuandika nyimbo zao wenyewe. Mmisheni wa tatu anafanya kazi na

Mpango wa Nne

## RWANDA

### Nchi Yenye Milima Elfu Moja

**Maandiko Matakatifu:** Luka 10:2-9

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake."*

*Luka 10:2*

**Kiongozi:**

Rwanda ni nchi ndogo yenye ukubwa sawa na Pori la Wanyama la Tsavo (Tsavo National Park). Ina eneo la maili mraba elfu kumi. Hupakana na nchi ya Burunda, Zaire, Uganda na Tanzania. Kuna wastani wa watu wapatao mia tano na hamsini maili moja mraba iwezayo kulimwa. Nchi hiyo ni yenye vilima, milima, mabonde na maziwa mengi yaliyoko katikati. Ni nchi ya kufurahisha sana na yenye hewa nzuri.

Rwanda ilipata uhuru wake kutoka kwa Ubeligiji katika mwaka wa 1962. Serikali ni ya kijeshi na Rais amechaguliwa kijeshi.

**Sehemu ya Kwanza:** Watu wa Rwanda

Nchi hiyo inayo makabila mawili makubwa, Wahutu na Watutsi. Wahutu ni themanini na tisa kwa mia (89%) ya idadi ya watu wote. Watu wengi ni wakulima na hulima mashamba yaliyo madogo, kwa sababu ya wingi wa watu. Ni watu wenye kufanya kazi kwa bidii. Tena tano kwa mia (5%) ya Wanyarwanda huishi mjini. Mji mkuu huitwa Kigali. Kwa muda wa miaka michache, watu wameanza kuishi Kigali wakijaribu kutafuta kazi.





amewakopesha pesa, na walipaswa kumrudishia zile pesa wakati ule. Veronika alijua kwamba hawakuwa na pesa za kutosha, na Abdullah atakasirika. Akijifanya kusahau mabadiliko yake ya asubuhi ile. Alikata shauri kumwambia kwamba mumewe alikuwa amekwenda mjini kwa haraka kwa sababu jamaa yake walikuwa wagonjwa. Alisahau kumwachia pesa, lakini ataweza kuzilete upesi atakaporudi. Kusema hivyo kungewapatia nafasi ya kutafuta pesa zingine.

**Sehemu ya Tatu:**

Ilikuwa siku ya soko na Elizabeti alikuwa akijitayarisha kupeleka mboga zake kuziuza sokoni. Aliwakuta marafiki zake wengi, wakasafiri pamoja. Veronika alikutana nao njiani. Walipocheka na kuzungumza njiani, Veronika aliwaambia jinsi alivyomdanganya Abdullah, lakini Elizabeti hakucheka na wengine. Alikuwa akifikiri juu ya dhambi nyingi ambazo alijua ni lazima ziachiliwe mbali ili wawe Wakristo wazuri.

Baadaye mboga zao ziliuzwa na wanawake hao wote walienda mahali pombe huuzwa kabla hawajaenda nyumbani. Veronika alijiunga pamoja na wengine na kujinunulia pombe yake, alifikiri, "Kweli, haitanidhuru nikinywa pombe hii. Marafiki zangu wote wanakunywa." Lakini alipoangalia upande mwingine, aliona kwamba Elizabeti hakununua pombe yo yote, lakini alikuwa akizungumza na mwingine.

Wanawake wengine walimwuliza Elizabeti kwa nini hakununua pombe. "Mimi ni Mkristo sasa," alisema akitabasamu.

**Sehemu ya Nne:**

Sasa tusome 2 Wakorintho 5:17 tena. Tulivyosikia juu ya marafiki wetu wawili Elizabeti na Veronika, je, twaweza kuona wazi kuwa Wakristo wapya wanahitaji kuviacha vitu vyote vya zamani ambavyo ni dhambi? Kusema uongo, magombano,

kutovumilia, unywaji wa pombe ni vichache vya vitu ambavyo vitaharibu maisha ya Mkristo. Unazo njia za zamani ambazo wapenda kuzitupilia mbali? Je, wengine waweza kuona kwamba umebadilika kwa sababu wewe ni Mkristo?

**Maombi:**

Tuombe ili kwamba kila mwanamke aliyeko hapa ataangalia katika maisha yake na kumwuliza Mungu kumsaidia kuwa Mkristo mwema.

Tuwaombee watoto wetu wanapoanza mwaka mpya kwa kurudi shuleni. Na hasa tuwaombee wale wanaoenda katika shule wanaposoma na kulala. Tumwombe Mungu ili ndipo awalinde na kuwaongoza muda ambao wako mbali kutoka kwa wazazi wao.





8. Si lazima kujua kila kitu kabla ya kujaribu kushuhudia.

9. **Eleza mtu mpaka awe na ujuzi wa wokovu wake binafsi.**

10. Eleza kwa urahisi juu ya **mpango wa wokovu.**

**Sehemu ya Nne:** Mpango wa Wokovu

1. Mwonyeshe mtu kwamba yeye ni mwenye dhambi na amepotea (Warumi 3:23).

2. Mwonyeshe kwamba hawezi kujiokoa yeye mwenyewe (Matendo 4:12).

3. Mwonyeshe kwamba Kristo ndiye awezaye kuokoa (Warumi 6:23).

4. Mwonyeshe kwamba Kristo atamwokoa ye yote ambaye ametubu na kuamini (Luka 13:5).

5. Mwonyeshe matendo ya yule ambaye ameishamwamini Kristo (1 Timotheo 6:11).

**Maombi:**

Tuombe ili Mungu atufanye kuwa mashahidi wake, kuanzia leo. Tuombe ili tupewe furaha ya milele.

4. Aliomba kila siku kwamba Mungu atampa nafasi kushuhudia na kumsaidia katika ushuhuda wake.

5. Aliandika orodha ya majina ya marafiki zake ambao hawakuwa Wakristo na kuwaombea kila siku. Aliwatembelea hao marafiki zake. Katika maisha yake ya Kikristo na maneno yake ya ushuhuda alijaribu kuwaongoza kwa wokovu katika Kristo. Alitaka watu wengine kuwa na furaha na amani katika mioyo yao kama yeye alivyokuwa.

**Sehemu ya Tatu:** Kuushinda Woga

Marafiki wengi Wakristo wa Mama Esta walikuwa na haya au na hofu katika kushuhudia habari za Kristo. Yafuatayo ni mambo ambayo yalimsaidia Mama Esta kushinda haya na hofu.

1. **Pendo.** "Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu" (1 Yohana 4:8).

2. **Kuzitegemea Ahadi za Mungu.** "Ingawa mtu anakwenda zake akilia, azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha, aichukuapo miganda yake" (Zaburi 126:6).

3. **Kuwa Mwaminifu Katika Maombi.**

4. **Kumvuta Mtu Mmoja** atakayesaidia kuwavuta wengine.

5. **Kuufuata Uongozi wa Roho Mtakatifu.** "Akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote" (Yohana 15:5).

6. **Kufahamu Kwamba Woga ni Dhambi.** "Kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi" (Warumi 14:23).

7. **Kufahamu kuwa kila mtu amepotea kabisa bila kuokolewa na Yesu.** "Sivyo, lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo" (Luka 13:5).





Mpango wa Pili

## MWANAMKE MPYA KATIKA KRISTO

**Maandiko Matakatifu:** 1 Petro 2:1-3

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Basi, wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote."*

*1 Petro 2:1*

**Utangulizi:**

Tumesoma katika Maandiko yetu Matakatifu kwamba ni lazima Mkristo aondoe vitu vingi katika maisha yake ikiwa anataka kukua katika neema yake Mungu. Atahitaji kuiondoa chuki, wivu, udanganyifu na kitu kingine cho chote ambacho kitaharibu njia yake mpya ya maisha. Atapenda kulisikia Neno la Mungu na kufikiria maana yake ili aweze kuwa kama Kristo. Leo, tutaona vitu ambavyo Elizabeti alivifanya ili kukua katika upendo wa Kristo.

**Sehemu ya Kwanza:**

Katika majuma yaliyofuata kuokolewa kwao, Veronika na Elizabeti walihudhuria Shule ya Jumapili na kanisani kwa uaminifu. Mara moja kila wiki walikuwa na darasa la wahoji ambalo liliongozwa na mchungaji. Darasa hili lilikuwa msaada mkubwa kwa sababu alieleza vitu vingi juu ya kuwa Mkristo na mshiriki wa kanisa la Kibatisti.

Elizabeti alifanya kazi kwa bidii nyumbani ili apate nafasi ya kuhudhuria darasa hili na ibada ya kanisa. Hakutaka kuchelewa hata siku moja. Veronika alikuwa na safari ndefu, na mara nyingi alichelewa kufika darasani au kanisani. Kwa hivyo ilikuwa vigumu kwake kufahamu kila kitu na kwa upesi alianza

kubaki nyumbani. Alikuwa na sababu nyingi ambazo alifikiri zilikuwa nzuri.

Safari ilikuwa ndefu sana, na alikuwa na kazi nyingi sana katika shamba lake. Zaidi ya hayo haikosi atahudhuria safari moja kila mwezi. Na hii itamtosha.

**Sehemu ya Pili:**

Mojawapo ya vitu vya kwanza ambavyo Elizabeti aliviona katika maisha yake mapya ni furaha katika kulisikia Neno la Mungu. Kila wiki aliweza kufahamu zaidi juu ya upendo wa Mungu. Hii ilimletea furaha kubwa. Hakuwa msomaji mzuri lakini aliweza kusoma kutoka katika Biblia yake kila siku. Baada ya kuvisoma alifikiri juu ya maana yake na katika wakati uliobaki wa mchana alijaribu kufanya jinsi Biblia ilivyomwambia kufanya. Dada yake alipotembelea alimwuliza kumsomea Biblia. Alijifunza shuleni na kwa hivyo aliweza kusoma vizuri. Mungu alikuwa mwema sana kwa kulipeleka Neno Lake kwa wote kulisoma na kulifuata.

**Sehemu ya Tatu:**

Elizabeti aliendelea kushangazwa na mabadiliko mengi ambayo yalikuwa yakifanywa pole pole moyoni mwake. Yeye alikuwa wa kwanza kuamka katika jamaa yake, aliamka asubuhi sana kabla ya mapambazuko. Siku yake yote ilijaa kazi nyingi sana ya kuwatunza jamaa yake, shamba na nyumba. Alianza kuufurahia utulivu wa asubuhi na kabla ya kuanza kazi nyingine aliomba na kuzungumza na Mungu.

Kwanza katika maombi yake alikuwa mwenye haya na wasiwasi. Hakujua jinsi ya kuomba. Kanisani mchungaji wake aliwaita Wakristo mbalimbali kuongoza maombi. Alipomwuliza kuongoza maombi aliogopa sana kwamba hakuna ye yote ambaye aliweza kuisikia sauti yake. Baada ya ibada mchungaji wake alimweleza kwamba alikuwa akizungumza na Mungu na





mmoja tu; kwamba Mwenyezi Mungu aliumba ulimwengu na kila kitu kilichomo. Mungu alimwumba mwanadamu ili awe na ushirika naye. Lakini alimpa mwanadamu hiari ya kumkubali au kumkataa Mungu. Mwanadamu alifanya dhambi. Alijitenga na Mungu. Kwa sababu Mungu ni Mtakatifu kabisa, hakuweza kuzikubali dhambi za mwanadamu. Walakini anampenda mwanadamu na anataka kumwokoa. Kwa hiyo, alimtuma Mwokozi ambaye ni Mwanaye Yesu Kristo kuwa dhabihu ya dhambi za mwanadamu. Katika Yesu Kristo tunaupata wokovu wa Mungu. Ni katika Yesu tu twaweza kurudishwa kwake Mungu. Yatulazimu tutubu dhambi zetu, tumkubali Yesu kama Mwokozi wetu na kumtii Mungu na kufanya kazi Yake katika ulimwengu Wake. Katika njia hii tunao ushirika kamili na Mungu na furaha na amani ulimwenguni na ahadi ya maisha ya milele katika Mungu.

**Sehemu ya Pili:** Kujitayarisha kwa Ajili ya Kushuhudia

Kabla ya mama Esta kutembelea jamaa hii, hawakujua kwamba Mungu atampa nafasi ya kumshuhudia mtu ye yote ambaye hakuwa Mkristo. Lakini alikuwa tayari kusema yote ambayo Mungu alikuwa amemfanyia. Alifahamu kazi yake kamili ulimwenguni ilikuwa kuwaleta wengine kumfahamu Kristo kama Mwokozi wao.

Alijitayarishaje kushuhudia?

1. Yeye mwenyewe ni Mkristo. Alijua moyoni mwake yote ambayo Mungu alimfanyia. Alikuwa amejifunza mpango wa Mungu kwa mwanadamu katika Shule ya Jumapili na Ushirika wa Wanawake. Tena amesoma mwenyewe binafsi.

2. Alisoma Biblia kila siku.

3. Alijifunza kwa moyo vifungu kutoka katika Biblia ambavyo vilimsaidia kumshuhudia mtu mwingine habari za Yesu.

JUNI

## Mpango wa Tatu

## USHUHUDA WA MTU BINAFSI

**Maandiko Matakatifu:** Mathayo 9:36-38

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache."*

*Mathayo 9:37*

**Utangulizi:**

Tumeumbwa kusudi tushirikiane na Mungu na kuwa kama vyombo vya kutumiwa kuwakomboa wenzetu. Ikiwa hatuwapendi wenzetu, basi hatumpendi Mungu hasa. Njia moja ya kushiriki vile tunavyompenda Mungu ni kushirikisha wengine pendo lake.

**Sehemu ya Kwanza:** Shahidi

Siku moja Mama Esta alikuwa akizuru nyumbani mwa mmojawapo wa watoto wa darasa la Shule ya Jumapili ambaye hakuhudhuria Shule ya Jumapili iliyopita. Mjomba wa mtoto alikuwa akitembelea nyumbani mle pia. Walipokuwa wakizungumza, Mama Esta alimwuliza mtu yule ni wapi anapokwenda kanisani. Alitaja madhehebu fulani. Halafu alisema, "Ni shule gani ambayo unasema? Je, wewe hufundisha Biblia?"

Naye Mama Esta alieleza kusudi la Shule ya Jumapili. Mtu yule alijibu, "Napenda kujifunza Biblia. Kanisa langu halifundishi Biblia. Je, kanisa lako ni la dini nyingine? Kanisa lako linafundisha nini?"

Hapo ndipo mama Esta alipata nafasi ya kumweleza yule mtu kwamba Wabatisti wanaamini kwamba kuna Mungu





Mungu naye aliweza kuyasikia yote aliyoyasema. Alianza kwa kumshukuru Mungu kwa wema wake. Na kwa upesi aliweza kuomba bila kuogopa hata kidogo.

**Sehemu ya Nne:**

Asubuhi moja wakati Elizabeti alikuwa akiponda mahindi alimwona Veronika akija. Baada ya kusalimiana, Veronika alianza kumwambia Elizabeti kwamba alifikiri hataweza kumaliza darasa la Wahoji kwa sababu alikuwa amekosa kuhudhuria mara nyingi na vilikuwako vitu kadha ambavyo hakuvifahamu na alihitaji msaada.

Elizabeti alifurahi kumsaidia na walipoketi katika kivuli alianza kumweleza Veronika mambo ambayo yalikuwa yamemtukia. Alikuwa ameishapata nguvu na maarifa mengi ya Mungu katika kuhudhuria kanisani kila mara alipoweza. Alijifunza njia nyingi za kuonyesha upendo wake kwake Kristo. Moyoni mwake alijua kwamba alihitaji kusikia na kujifunza Neno lake Mungu. Shida za kila siku zilimalizwa kwa kuitumia Biblia yake na kufuata shauri lililoandikwa ndani yake. Na sikuzote alimwambia Veronika, alijisikia akiwa na hitaji la kuzungumza na Mungu katika maombi.

Wakati Veronika alipoondoka alikuwa na shukrani kwa rafiki yake Elizabeti na alijua kwamba yeye vile vile lazima akue katika ushirika wake wa Mungu. Atafanya hivi kwa kuhudhuria kanisani kwa uaminifu, kujifunza Neno la Mungu, na kumwomba Mungu kila siku.

**Kiongozi:**

Wakristo wote wanahitaji kuzitumia njia ambazo Elizabeti alitumia ili wakue katika neema ya Mungu. Kristo anapoishi ndani yako, lazima uwe na ushirika naye kila siku. Yeye ni rafiki yetu na atatusaidia wakati wo wote tukimwomba. Lakini lazima tuwe na juhudi naye atatupa nguvu. Unapoabudu katika

nyumba ya Mungu hupokea nguvu kwa maisha ya kila siku. Unapolisoma Neno lake kila siku na kuzungumza naye, utajazwa na furaha na amani.

**Maombi:**

Tumwombee kila mwanamke aliyeko hapa leo ili aone hitaji la msaada wa Mungu na kuitumia kila nafasi kushirikiana naye Kristo.

Tuiombee kazi ya Kibatisti kati ya Wamaasai. Tuwaombee wamisheni Carl Hall na mke wake Gerry wanaofanya kazi kati yao. Tuombe ili Mungu afanye kazi katika mioyo ya Wamaasai.





**Maombi:**

Kila mama aombe kwa kimya kwa muda mfupi kwamba Mungu atamwongoza siku kwa siku katika kuwatunza watoto wake.

Tuwaombee Wabatisti katika nchi ya Uganda. Omba ya kuwa wataweza kupata mahitaji yao ya maisha. Omba kwa Moses Ochwa, Kinara wa Jumuiya yao. Wasaidie kukaa salama na kuhubiri na uwezo wa Mungu.

"Ndiyo, nayapenda maua yote yanayoonekana kuwa mazuri, miti ambayo tuko nayo," Daudi alisema.

"Je, wapenda kumshukuru Mungu kwa kutupa vitu vizuri vya kufurahia?" maana aliuliza.

"Ndiyo, napenda," Daudi alijibu. Aliinamisha kichwa chake na kusema, "Asante Mungu kwa vitu vizuri ambavyo umetupa, zaidi, maua na miti na hata mdudu huyu ambaye hula mbu."

Daudi alianza kujifunza kutoa shukrani kwa ajili ya viumbe vya ajabu na vitu vizuri ambavyo humzunguka. Baadaye ataweza kukubali kwa urahisi tofauti iliyoko kati ya watu kwa sababu anajua kwamba Mungu aliwaumba hivyo.

**Sehemu ya Tano:** Kufundisha Tabia Njema

Katika kuwafundisha watoto wetu tabia njema, hizi ndizo baadhi za sifa ambazo twataka kuwafundisha watoto wetu:

1. Kuwaheshimu wengine, na kuheshimu haki na mali zao.
2. Ukweli na uaminifu katika matendo ya kila siku.
3. Ujitahidi katika kumaliza kazi zake zote.
4. Hekima katika kukata shauri mwenyewe.
5. Ustadi wa akili wa kuweza kukata shauri baina ya mambo mawili yaliyo muhimu.
6. Upendo ambao huwafikia watu wa mataifa na nchi mbali-mbali.

Ni dhahiri kwamba sifa kama hizi haziwezi kusitawishwa kwa siku moja, lakini pole pole kwa muda wa miaka kadha. Watoto hawazaliwi wakiwa na akili ya tabia njema, lakini wanapata akili hii katika uongozi ambao wanapata nyumbani na kutoka hali ya maisha ambayo wazazi wao huwapa.





Mpango wa Tatu

## MWANAMKE MPYA NYUMBANI

**Maandiko Matakatifu:** Wakolosai 2:6-7

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Basi, kama mlivyompokea Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye."*

*Wakolosai 2:6*

**Utangulizi:**

Sasa hamna budi mmeisha wafahamu Elizabeti na Veronika vyema. Leo tunaona jinsi wanavyoendesha njia za Kikristo nyumbani. Kama tujuavyo mengi kuhusu Kristo, ndivyo tutapenda atuongoze katika juhudi zetu zote. Tunahitaji kutembea katika Kristo kila dakika ya kila siku. Tunaposhindwa kufanya hivyo, tutakosa kuzungumza naye kila siku na mara tunasahau kuwa kama Yeye. Leo wakati tunaposikia habari za wanawake hawa wawili, peleleza uone ikiwa wewe ni kama mmojawapo wa wanawake hawa.

**Sehemu ya Kwanza:**

Veronika alipokuwa anamaliza kazi shambani alikuwa akifikiri sana juu ya maneno ambayo mchungaji Peter aliyasema kanisani Jumapili. Alisema kila mama anapaswa kuwafundisha watoto wake njia zake Mungu. Ndivyo, lazima aanze kuwaambia watoto wake njia zake Mungu. Baadaye ataanza kuona kwamba watoto wake watahudhuria kanisani pamoja naye. Wakati mwingine watoto wawili wakubwa walienda naye, lakini alikuwa mchovu saa zote hata hakujali kuwachukua wale wadogo. Tena, alifikiri, wataweza kujifunza habari za Yesu watakapokuwa wakubwa.

Aliingia ndani ya nyumba akaanza kupika chakula kwa jamaa yake. Watoto wake wakubwa walipofika kutoka shuleni na vile mumewe alipofika kutoka kazini wote wataonekana wakiwa wenye njaa sana. Hakuchukua nafasi ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya chakula lakini alianza kukipakua mara tu walipofika. Usiku ule baada ya kila mmoja kulala, wakati alipokuwa akifumba macho yake aliwaza "Kesho nitajaribu kuwaambia juu ya Yesu na nitawafundisha njia za Mungu."

**Sehemu ya Pili:**

Elizabeti naye pia alikuwa na kazi nyingi za kufanya kila siku. Pamoja na kuwatunza watoto, mamaye aliyekuwa mgonjwa aliishi nao. Mara kwa mara kulikuwako na ndugu ambao walikaa hapo pia. Watoto wake walipokuwa wakiamka kila asubuhi walimsikia akiimba mojawapo ya nyimbo mpya ambazo alikuwa amejifunza kanisani. Siku moja alipokuwa akiimba, alishangaa wakati mtoto wake wa umri wa miaka mitano alipoanza kuimba pamoja naye. Mara nyingi waliimba walipokuwa wakifanya kazi nyumbani au shambani.

Alijaribu sana kufuata shauri la mchungaji wake. Alijua kwamba hana budi kuwafundisha watoto wake Neno la Mungu ili kwamba wataweza kumpenda Yesu jinsi yeye mwenyewe alivyompenda. Mara nyingi aliwaambia vitu ambavyo alijifunza katika darasa la wahoji. Na kila Jumapili aliwasaidia wote kuoga na kujitayarisha kwenda Shule ya Jumapili. Waliweza kujifunza mengi kutoka masomo yao. Alijaribu kuwa mwenye upendo na kuleta uhusiano mwema kwa kila mtoto wake.

**Sehemu ya Tatu:**

Muda mfupi baada ya kuwa Mkristo, Elizabeti alizungumza na mume wake, akamweleza kwa njia ya unyenyekevu kwamba Yesu alikuwa amekuja moyoni mwake na alipaswa kufanya vile Neno la Mungu lilivyosema. Alimwomba afike kanisani pamoja





**Sehemu ya Tatu:** Kufundisha Juu ya Ukarimu

Mama alirudi nyumbani baada ya kutembelea jirani yake siku moja na kusema kwa mtoto wake, "Marko, mtoto wa jirani yetu ni mgonjwa na baba yake hana kazi. Unafikiri tutafanya nini?" Kijana alisema, "Tunaweza kumpa mayai. Kuku zetu wanataga mayai mengi sana."

"Hilo ni wazo nzuri," mama alisema.

Jane alisema, "Ninayo motokaa ambayo nimeitengeneza kutoka kwa sanduku. Pengine atapenda kucheza nayo."

Mama alisema, "Nafikiri kwamba atapendezwa sana."

Petro mtoto mdogo alisema, "Nitamchorea picha." Kwa hiyo kila mtoto alikuwa na sehemu ya kumsaidia Marko na kujifunza jinsi ya kusaidiana. Mama aliweza kuvichukua vile vitu vyote na kumpa Marko, lakini kwa kuwaacha watoto wake washirikiane katika kuutoa msaada, aliwafundisha somo muhimu.

**Sehemu ya Nne:** Kufundisha Kutoa Shukrani

"Mama tazama mdudu huyu ambaye nilimpata," Daudi alisema. Mama yake alisema, "Ndivyo, nimeona. Huyu ni mdudu aitwaye vunjajungu. Mdudu huyu hula mainzi na mbu, kwa hiyo, ni mdudu mwenye msaada."

Daudi alisema, "Lakini mdudu huyu anaonekana kuwa wa ajabu?"

"Ndivyo," mama alisema, "Hivyo ndivyo jinsi Mungu alivyomwuumba. Wakati uangaliapo vitu vingi mbalimbali ambavyo Mungu aliviumba, waweza kujua kwamba Mungu ni mkuu sana kwa sababu ameviumba vitu vingi vya ajabu na anapenda vitu mbalimbali. Je, wafurahi kwamba Mungu aliviumba vitu vingi vya kutufurahisha?"

kwa kununua nguo za bei ya juu ambazo zingetumiwa vizuri kwa chakula cha watoto. Heri wazazi wawe waaminifu kwa Mungu na kwa watu wengine.

**Sehemu ya Pili:** Tuwafundisheje Uaminifu?

Mama na mtoto wake wa miaka mitano walikwenda dukani. Mama alinunua mkate, akaweka pesa kwenye meza mbele ya karani, ambaye aliziona, lakini alichelewa kuzichukua haraka. Yule mama aligeuka kuangalia kitu kingine mle dukani. Kisha alimwita mtoto wake wa kike na hapo wakaondoka dukani. Alipoushika mkono wa mtoto wake, ili wavuke barabara ya mjini, mtoto wake alikuwa na shilingi mkononi mwake. "Hii shilingi uliipata wapi?" mama alimwuliza mtoto. "Dukani", mtoto alijibu.

"Je, hizi ndizo pesa nilizoweka mezani kule dukani kulipia mkate?" mama alimwuliza mtoto. "Lakini yule karani hakuzipenda; hakuipokea shilingi," mtoto alisema. "Pesa hizi ni za mwenye duka. Umeziiba kwa kuzichukua. Tutarudi mpaka dukani. Yakulazimu umpe karani pesa hizi na kumwambia kwamba umesikitika kwa kuzichukua pesa hizi," mama alisema.

Kama mtoto angekuwa mkubwa na kufahamu ni nini maana ya kuiba, mama yake angemwambia: "Wajua kuwa ni vibaya kuiba. Ikiwa huzirudishi pesa hizi, utakuwa na makosa ya kutokuwa na furaha. Utafanya nini?" Kama mtoto angejibu, 'Kazirudishe pesa hizo dukani,' mama yake angeenda naye kuzirudisha pesa hizo, na kumwacha mtoto aeleze kwa karani na kuzirudisha pesa. Ikiwa mtoto hana ufahamu kwamba ni lazima pesa zirudishwe, mama amsaidie mtoto wake kwa njia ya upole mpaka atakaposadiki haya yote.

Huu ni mfano mkubwa wa kufundisha tabia njema. Tabia njema hufundishwa siku kwa siku kwa vitendo vya kila siku.





naye na akaomba moyoni kwamba mumewe awe Mkristo pia. Hamisi hakutaka kwenda kanisani wala kuwa Mkristo, lakini aliona badiliko lilipoonekana katika maisha ya Elizabeti. Yeye aliona badiliko katika watoto wao pia. Kwa hivyo, aliweza kutulia katika maombi ya mkewe.

Ombi moja lisilo la kawaida lilikuwa wakati maalum wa chakula. Haikuwa desturi kwa jamaa kula wote pamoja, lakini Elizabeti alijaribu kufanya hivyo mara nyingi. Kabla ya kula chakula alikuwa akianza kwa maombi ya kumshukuru Mungu kwa chakula walichopata. Kwa upesi Bwana alianza kuinamisha kichwa chake pamoja na mke wake alipoongoza katika maombi ya kutoa shukrani. Hata alianza kujisikia kuwa anayo tofauti ndani. Na Jumapili moja, Elizabeti alipomwalika kwenda naye (alikuwa akimwalika kila Jumapili) aliende. Furaha ilimjaa roho yake na alifahamu kwa nini Wakristo wanapaswa kuwa kielelezo cha Kristo nyumbani.

**Sehemu ya Nne:**

Kunazo njia nyingi ambazo twaweza kuonyesha upendo wa Mungu wakati tufanyapo kazi kila siku nyumbani mwetu na mashambani. Kitu kimoja ambacho ni lazima tukiweke akilini mara nyingi ni "kutembea katika Kristo." Kazi hii siyo rahisi, na ni lazima tuombe kwamba Mungu atatuongoza sisi na kutupa nguvu na ujasiri kufanya hivi.

Tumeona njia chache ambazo Elizabeti na Veronika walichagua kufuata. Je, uliona kwamba Veronika alichukua njia rahisi? Twafanya hivi mara nyingi kwa kusema kesho tutaanza. Lakini mara nyingi kesho haifiki kwa kweli. Hatuwezi kukawia kufanya wajibu wetu wa Ukristo. Watoto wetu lazima wajifunze leo, kabla hawajakuwa wakubwa na kujifunza njia nyingine ambazo si za Kikristo. Hata mtoto mdogo sana anaweza kuanza kusikia juu ya upendo wa Mwokozi wetu. Elizabeti alikuwa mwaminifu kwa kuwasaidia jamaa yake kufahamu njia za

Kristo. Alikuwa akifanya jinsi Mungu alivyotaka afanye sikuzote. Aliishiriki imani yake na mumewe na watoto wao.

**Kiongozi:**

Wanawake wote wana wajibu wa kutunza nyumba zao na jamaa, lakini wanaweza kufanya vitu hivi vyote katika njia nyingi kuonyesha upendo wa Mungu. Ikiwa watalegea kwa kuwa wachovu sana na kuacha kuwasaidia jamaa zao kufahamu njia ya Mungu, itakuwa kazi ngumu sana. Lakini tukianzisha kila siku kwa msaada wa Mungu, twaweza kutumia kila nafasi kuwaonyesha wapendwa juu ya Yesu na upendo wake. Je, wewe hujaribu kila siku kushirikiana imani yako pamoja na jamaa yako? Ebu tunapoomba, tumwulize Mungu kutupa nguvu.

**Maombi:**

Tuombe kwamba kila mwanamke na mzazi atamleta Kristo katika nyumba yake na kushirikiana pendo lake pamoja na wengine wote.

Tuiombee kazi ya Kibatisti iliyoko Bukoba. Omba Mungu kuwaongoza Bw. na Bi. Whitson na wachungaji wote wa eneo hili.





Mpango wa Pili

## USHUHUDA KATIKA KUWAFUNDISHA WATOTO

**Maandiko Matakatifu:** Kumbukumbu la Torati 6:4-7

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo."*

*Kumbukumbu la Torati 6:7*

**Sehemu ya Kwanza:** Sababu ya Kuwafundisha Watoto

Kama tunao watoto au hatuna, wengi wetu tumezungukwa na watoto. Tunayo kazi ya kuwapenda na kuwafundisha. Ikiwa Mungu amekupa wewe watoto, mojawapo ya kazi yako kubwa katika maisha ni kuwafundisha upendo na amri zake Yesu Kristo. Kuwa Wakristo maana yake ni kufikiria maisha kama kipawa cha Mungu, kukumbuka kwamba wakati unapaswa kutumiwa vizuri, kuwa mwaminifu, mwema, mvumilivu na kuwa na upendo.

Je, tutaweza kuyafundisha mambo haya mema kwa watoto wetu? Watoto hujifunza mengi kutoka kwa matendo mema kuliko kutoka kwa mafundisho matupu. Kwa hiyo ni lazima tuyatekeleze mambo hayo mema sisi wenyewe. Watoto hujifunza kusema uwongo ikiwa wanawasikia wazazi wao wakisema uongo juu ya umri wao ili waweze kuwapatia nafasi katika shule. Hujifunza kusema uwongo wakati wamsikiapo baba yao akimwambia rafikiye, "Sikuenda kazini leo. Nilimwambia mkubwa wangu kwamba nilikuwa mgonjwa, lakini kwa kweli nilitaka kuwatembelea marafiki zangu." Wanajifunza kudharau utakatifu wa maisha wakati waonapo baba yao akija nyumbani akiwa mlevi; mama yao akiharibu pesa

Wakati tuendapo shambani kupanda mbegu za mahindi, twaweza kupanda mbegu za uzuri na upendo wa Yesu Kristo njiani. Yesu alituambia tuwe chumvi ya ulimwengu. Kila chakula chahitaji chumvi kidogo ili kiwe na utamu. Wakati tukutanapo na watu siku kwa siku tunawapa "chumvi" kidogo ya injili mpaka watakaposadiki kwamba tunacho kitu ambacho wao hawana. Halafu twaweza kushirikiana nao kwa hakika ule upendo wa wokovu na Yesu Kristo.

**Maombi:**

Omba kwa kila mmoja wenu atakuwa na nguvu katika kumshuhudia habari zake wiki hii.

Omba kwa kazi mpya katika Rumuruti. Omba kwa ajili ya Waturkana ili waweze kumwamini Yesu. Omba kwa wamisheni Jim Green na mke wake Ruth Ann.



APRILI

Mpango wa Nne

## MWANAMKE MPYA KATIKA JAMII NA KANISANI

**Maandiko Matakatifu:** Wagalatia 6:9-10

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho."*

*Wagalatia 6:9*

**Utangulizi:**

Wakati tunapoendelea kukua katika neema na wema wake Mungu, tutautambua wajibu wetu katika vijiji, jamii na kanisani mwetu. Tunapaswa kuwahurumia wale tunaokutana nao kila siku. Kama tusomavyo katika Maandiko Matakatifu tusilegee katika kufanya vitendo vizuri. Kila siku tunakuwa mashahidi kwa marafiki na majirani wetu. Aina ya ushuhuda wetu hutegemea matendo mema na uaminifu kwa Mungu.

**Sehemu ya Kwanza:**

Elizabeti alikuwa na huruma iliyokua kwa marafiki zake. Mara kwa mara wanawake walimtembelea wakati wa jioni. Mara nyingi walikuwa na mazungumzo ya kawaida, lakini kwa vile Elizabeti alikuwa Mkristo, wakati mwingi aliweza kuyaleta mazungumzo yanayohusiana na Yesu na mambo ambayo amejifunza katika kanisa. Wanawake wengi walikuwa Waislamu na wengine hawakuwa na dini hata kidogo. Siku ya Ushirika wa Wanawake na siku ya Jumapili alihakikisha ya kuwa ameishawaalika wanawake wale marafiki zake wote kufika pamoja naye. Wakati mwingine waliweza kufika na kushiriki katika ibada. Alijua kwamba ni wajibu wake wa kutembelea na kuzidi kuwaambia wengine habari za Yesu.

Veronika alikuwa akijifunza pia. Ilikuwa vigumu sana kwake kuwaambia wengine habari za Yesu. Wakati mwingine rafiki zake walimcheka alipokuwa akiwaambia kuwa alihudhuria kanisani.

Wakati walipokuwa na furaha kwa mazungumzo, yeye hakuenda kanisani lakini alijua moyoni mwake kwamba ni vibaya na alihuzunishwa na jambo hilo.

**Sehemu ya Pili:**

Jinsi majuma yalivyozidi kuendelea ndivyo Elizabeti alivyoendelea kujifunza njia ambazo anaweza kuwaonyesha wengine upendo wa Mungu. Alikuwa mshiriki mwenye bidii sana wa Ushirika wa Wanawake na kwa utumishi wa jamii aliweza kufanya mengi kwa wengine. Marafiki zake ambao hawakuwa Wakristo walipozaa watoto aliona kama huo ndio wakati mzuri wa kuwatembelea na kuwapa kijitabu chenye maelezo ya njia ya wokovu ndani yake na vifungu kutoka katika Biblia.

Nafasi nyingine ya kushuhudia ilitokea wakati kulipotokea kifo katika jamii. Ilikuwa desturi kwa wakaaji wa vijiji vile kwenda nyumbani mwa wale jamaa na kulia pale pamoja nao kwa muda wa siku nyingi. Elizabeti alijua kwamba hii haikuwa njia ya Kikristo. Alichukua chakula kama mkate, ndizi au ugali na kuwapelekea wale jamaa waliofiwa. Halafu alikaa pale nyumbani akipika chakula kwa jamaa waliofika kwa mazishi, au kusaidia jinsi awezavyo. Alipopata nafasi ya kuwafariji alisoma kutoka katika Biblia yake, na kueleza kwamba Mungu ni Mungu wa upendo na angewapa nguvu kama wangeweza kumwomba. Wakati mwingine marafiki zake walimwuliza amwombe Mungu kwa ajili yao.





Lydia alitoka kijijini mwake kwenda mjini mahali ambapo mumewe alipata kazi. Mle mjini hakumjua mtu ye yote. Hakuweza kuzungumza lugha ya Kiswahili sawasawa. Mumewe aliondoka kwenda kazini na kushinda kule mchana kutwa na usiku aliendа nje kwa matembezi pamoja na marafiki zake. Mwanamke huyu alijiona mpweke na mwenye huzuni. Siku moja alimkuta Mary dukani. Mary ambaye alikuwa Mkristo alihusika sana na jirani zake. Aliweza kutambua hali ya mwanamke huyu kwa kuuangalia uso wake na kujua kwamba kitu fulani kibaya kimetendeka. Mary alizungumza naye. Alimwuliza juu ya jamaa yake, mahali alipoishi, muda gani alioishi mjini.

Lydia alikuwa na furaha kuzungumza. Mary alimkaribisha Lydia nyumbani kwake kwa chai. Walianza kufahamiana na kuwa marafiki. Mary alisikiliza shida zote za Lydia. Mary alijitoa kumfundisha Kiswahili na kumjulisha kwa wengine ambao walikuwa jirani zake. Alimkaribisha Lydia kwenda naye kwa ibada na kwa Umoja wa Wanawake Wabatisti Waenezao Injili. Baadaye, Mary aliwachukua jirani kwenda kumtembelea Lydia. Wanawake walianza kutembeleana. Mary alimwuliza mumewe kwenda naye kumzuru Lydia na mumewe ili wawakaribishe kwenye ibada katika kanisa lao. Kwa upesi Lydia alikuwa na marafiki wengi wapya. Lakini Mary hakumsahau Lydia. Aliendelea kumtembelea na kumpa moyo wa kuendelea.

**Sehemu ya Nne:** Chumvi ya Ulimwengu

Wakati unapokwenda sokoni, kuteka maji au kufanya kazi shambani, unaweza kushuhudia. Mara nyingi twasimama kuzungumza na marafiki au jirani tukiwa njiani. Je, tunaanza kumsifu Mungu, au kunung'unika juu ya kazi yetu au taabu zetu? Mara nyingi wakati tuchekapo au kuimba tukiwa njiani, watu wengine hufanywa kuwa wenye furaha sana wanapoona furaha yetu. Furaha ni kitu cha kuambukiza.

Unaanzaje siku yako? Ikiwa tunamwomba Mungu kabla ya kutoka kitandani asubuhi, hii itatusaidia kujitayarisha kwa ibada ya kumwabudu Mungu mchana kutwa.

Kusoma sehemu za Biblia kama Zaburi 5, 8, 11, 19, 23, 25, 46, 62, 90; I Yohana 3; I Wakorintho 12, na maombi ya jamaa asubuhi na mapema hutusaidia sisi kuujua umoja na Mungu na kushirikiana kila mtu na mwenzake.

**Sehemu ya Pili:** Kazi Yako

Kwa sababu kazi ni takatifu, yatulazimu kuipanga kazi yetu vizuri, ili impendeze Mungu. Wakati usafishapo sahani na maji moto kwa kutumia sabuni, je, wasadiki kwamba hii ni njia ya kushuhudia? Kwa kuwa wakati usafishapo sahani vizuri, waweza kuwazuia jamaa yako kuwa wagonjwa, yaani maana yake ni kuwapa nguvu za kuabudu na kumshuhudia Mungu. Wakati ufagiapo nyumba yako waweza kuomba kwamba Mungu atayasafisha maisha yako kila siku. Wakati unapozisafisha nguo zako au kuzipiga pasi, waweza kuomba kwamba Mungu ataweka roho ya Ukristo katika yule mvaaji ili awe kama vile usafi unavyoonekana nje ya nguo zile.

Unapaswa kutayarisha kazi yako ili kwamba utakuwa na wakati wa kucheza na kuwafundisha watoto wako, kuzungumza na mume wako, kujifunza Neno lake Mungu na kuonyesha fadhili na msaada kwa jirani zako.

Usafi na utumiaji bora wa pesa ni njia za ushuhuda, kwa maana mambo hayo yanazuia kugombana, huzuni na ugonjwa.

**Sehemu ya Tatu:** Kuushiriki Wokovu

Kunazo njia nyingi za kushirikisha Habari Njema za Mungu. Watu wote wanatafuta upendo na wema. Watu wanataka kuona matokeo ya Habari Njema, siyo kusikia habari yake tu. Kwa hiyo, mfano ulio na uhai ni bora sana kuliko hotuba, hata ikiwa kufundisha kwa kutumia hotuba kunahitajika pia.





**Sehemu ya Tatu:**

Basi kwa kuwa walikuwa wamekuwa washiriki wa kanisa la Kibatisti kwa kitambo, kulikuwako na vitu vingi ambavyo Veronika na Elizabeti wangefanya. Elizabeti aliombwa kufundisha darasa la watoto katika Shule ya Jumapili wakati mwalimu wa darasa hilo alipokuwa ameenda kuwatembelea jamaa. Alikuwa hajafundisha hapo mbeleni, lakini mwishowe alikata shauri kujaribu kufanya vizuri awezavyo.

Kanisa lilipoanzisha madarasa ya kuwaelimisha viongozi wa makanisa ya jumuiya yao kwa muda wa siku tatu, Veronika na Elizabeti walijitoa kuwasaidia kupika chakula kila siku. Ingawa walifanya kazi zaidi ya kiasi kwao nyumbani, walikuwa na furaha kuwa na sehemu katika kazi ya Mungu.

Katika Ushirika wa Wanawake walikuwa na nafasi ya kusoma sehemu katika masomo. Wakati ulipofika kwa majadiliano kati yao juu ya matatizo na mahitaji yao, walitoa mawazo bila kuogopa kusema jinsi walivyojisikia. Kila mwezi walienda pamoja na wengine wa kundi lao kuwatembelea wagonjwa au washiriki ambao hawakuhudhuria kwa muda mrefu.

**Sehemu ya Nne:**

Katika kumaliza mipango yetu juu ya Mwanamke mpya, ebu tuangalie katika Maandiko Matakatifu yetu ambayo tumejifunza. Kwanza soma 2 Wakorintho 5:17. (Halafu waite wengine kueleza maana yake). Je, umekuwa mtu mpya katika Kristo? Ikiwa umeishakuwa mtu mpya, basi, umejaribu kuvitoa vitu vibaya ulivyokuwa navyo katika maisha yako ya zamani?

Sasa soma 1 Petro 2:1-3. (Mpate mtu mwingine awe tayari kusoma.) Je, unataka kulisikia Neno la Mungu kwa kweli na kujifunza kutoka kwake? Ikiwa unataka, utakuwa mwaminifu

kuhudhuria kanisani kumwabudu Yeye. Utasoma Biblia yako, au kumwomba mtu mwingine kukusomea kila siku ili kwamba utaweza kukua katika neema ya Mungu.

Sasa funua kutoka Wakolosai 2:6-7 na tutasoma sisi sote pamoja. Je, wewe hutembea katika hatua za Kristo? Je, umekuzwa juu yake? Ni lazima uyafuate mafundisho yake katika yale yote uyafanyayo. Je, nyumba yako yaonyesha kwamba unampenda Mungu?

Mwisho, ebu tusome tena Maandiko Matakatifu yetu ya leo, Wagalatia 6:9-10.(Yasome wewe). Ikiwa tumelifuata Neno la Mungu na kuvifanya vitu hivi vyote vingine na kukua katika upendo wake, hatutachoka kuwasaidia wengine. Utatumia kila nafasi kuwasaidia marafiki zetu na wataona kuwa wewe u Mwanamke mpya.

**Maombi:**

Uliza kila mmoja aliyeko kuinamisha kichwa. Ombeni maombi mafupi kutoka kwa kila mmoja ambaye anataka kuomba msaada kutoka kwa Mungu wakati watembeapo katika hatua zake na kuishi kila siku kwa ajili ya Kristo.

Na tuiombee kazi ya Kibatisti katika vijiji vidogo vilivyoko nje ya mji wa Dar es Salaam. Tuombe ili kwamba watu wengi waweze kumwamini Yesu. Na tuombe kwa makanisa mengine ya Dar es Salaam ili yawe na nguvu ya kushuhudia.





Mpango wa Kwanza

## USHUHUDA NYUMBANI

**Maandiko Matakatifu:** Isaya 60:1-2

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana; usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi."*

*Yohana 9:4*

**Utangulizi:**

Maisha ni matendo mengi ambayo hufanywa siku kwa siku. Haya yenyewe huonekana kama siyo jambo muhimu, lakini yakitiwa pamoja hufanya maisha kuendelea vizuri sana na kutupa sisi furaha. Wakati mwingi tunachoshwa na kazi ya kila siku, lakini tufikiriapo kwamba Mungu alitupa sisi kazi, na kazi hii ni takatifu kwake, basi cho chote tutendacho, twatenda kwa ajili yake.

Ikiwa Mungu amekubariki wewe pamoja na jamaa yako, mnayo madaraka kwake Mungu kuwatunza wale jamaa. Huu ni ushuhuda wa kila siku. Wawezaje, kuwa na upendo, uvumilivu, ufahamu na nguvu za kuwa shahidi katika vitendo vya kila siku?

**Sehemu ya Kwanza:** Anzisha Siku Yako Pamoja na Mungu

Nisaidie nijazwe na furaha ya siku mpya, na nafasi mpya.

Nipe juhudi katika kazi yangu leo.
Nisaidie niwe mvumilivu, mwenye upendo wa heshima.
Kutokea dakika za kwanza za asubuhi nataka ufahamu, furaha na nguvu viende mbele kuniweka mimi karibu nawe kila saa ya siku hii."

nitakuwa Mkristo." Tena, aliambiwa kwamba Mungu alitaka yeye aamini katika Yesu na ataokolewa. Mjumbe aliondoka kwa huzuni.

Wiki iliyofuata wamisheni walipofika, mjumbe alikuwa wa kwanza kufika pale. Alisema, "Kwa wiki nzima nimekuwa nikimwomba Mungu wenu kunisaidia nifahamu. Sasa najua---kwanza ni lazima nijitoe mimi mwenyewe kwake Yesu. Halafu nitakitoa cho chote nilicho nacho na kuwa na amani moyoni mwangu."

Yule mjumbe alijifunza somo ambalo sisi sote tunahitaji kujifunza---kujitoa sisi wenyewe.

**Maombi:**

Kwanza, mwe na maombi mafupi, mkimwuliza kila mmoja aliyeko kuyapeleleza maisha yake binafsi na kuona ikiwa kwa kweli amejitoa mwenyewe kabisa kwa Yesu.

Tuwaombee Wabatisti wa nchi ya Zimbabwe. Omba ili waweze kujenga tena kazi iliyo haribika wakati wa vita.

**Wimbo wa Kufunga:** "Yote Namtolea Yesu"



MEI

Mpango wa Kwanza

## KUHUDHURIA KANISANI

**Maandiko Matakatifu:** Zaburi 100

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Mtumikieni Bwana kwa furaha; njoni mbele zake kwa kuimba; Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake."*

*Zaburi 100:2-3*

**Kiongozi:**

Kwa muda wa miezi miwili tutakuwa tukijifunza njia ambazo twaweza kuwa kama Kristo. Kunazo njia nzuri nyingi ambazo twaweza kupata kina cha maisha yetu ya kiroho. Nazo ni: Uaminifu wa kuhudhuria kanisani, maombi ya kila siku, mafunzo ya Biblia ya kila siku, uwakili wa binafsi unaoendelea, na ushuhuda wa Kikristo. Ni nguvu za Mungu na usaidizi wake zinazoendeleza asili yetu ya kuwa kama Kristo.

Leo tutaona majibu ya maswali mengine ambayo yameulizwa na Wakristo ambao wana tamaa ya kukua katika upendo wa Mungu. Je, kuhudhuria kanisani ni jambo muhimu sana. Kwa nini?

**Sehemu ya Kwanza:**

Wengi wetu huenda kanisani mara nyingi kama tuwezavyo. Ebu tuanze kwa kuuliza swali. Kwa nini unahudhuria kanisani, au Ushirika wa Wanawake? (Wangojee wanawake wengine wajibu. Ikiwa hakuna atakayesema kitu cho chote, mwite mmoja wao aseme kwa nini anahudhuria.) Nafikiri sisi sote tutakubali kufika kanisani kumwabudu Mungu na kupokea nguvu za kuishi kila siku.

Kanisa ni kundi la waamini waliobatizwa. Si lazima kuwa na mjengo wa kanisa ili ndipo tuwe na kanisa. Pengine wengi wenu mmeenda kanisani katika nyumba ya mtu au nje kwenye mti. Kanisa ni kundi la watu wanaomwabudu Mungu wakiwa pamoja. Mungu anajua kwamba twahitaji kukutana pamoja kushiriki katika upendo. Kwa kuhudhuria kanisani twaweza kushirikiana pamoja na Wakristo wengine. Wakati tufanyapo hivyo, mioyo yetu hujazwa na uwezo na umbo Lake. Tunapozidi kujazwa na upendo wake Mungu tutakuwa na ufahamu mwingi kuhusu wajibu wetu wa kumtumikia Yeye. *Kanisa ni mahali pa kuabudu.*

**Sehemu ya Pili:**

Sababu nyingine ya kuhudhuria kanisani ni kwa kulisikiliza Neno la Mungu. Twabarikiwa kuwa na viongozi wazuri katika makanisa yetu ambao wameongozwa na Mungu. Kila Jumapili asubuhi waalimu wetu wa Shule ya Jumapili wanayo masomo katika Mafunzo ya Biblia. Wamefanya kazi na kujifunza kwa bidii kutufundisha sisi mengi juu ya Neno la Mungu. Katika Ushirika wa Wanawake tuna mipango mizuri ambayo imetayarishwa kwa ajili ya kufundisha. Lakini kuyapokea mafundisho haya, lazima tuhudhurie, tusikilize na halafu tuchukue yale tumesikia mioyoni mwetu.

Wachungaji wetu ni watu waliochaguliwa na Mungu ambao hutuhubiria kwa uwezo wake. Ikiwa tutasikiliza na kufuata mafundisho yao, tutakua katika neema ya Mungu kila siku. Ni katika uaminifu wetu tu, tuwezapo kutembea pamoja na Mungu kila siku. *Kanisa letu ni mahali pa kulisikiliza Neno la Mungu.*

**Sehemu ya Tatu:**

Twajifunza njia nyingi za kufuata mafundisho ya Kristo kwa kuhudhuria kanisani. Katika maombi yetu ya ibada twajifunza





tuwezavyo kufanya. Kwa kutoa yote, ni lazima tuitumie miili kama amana kutoka kwa Mungu. Katika Warumi 12:1 husema ya kuwa "tuitoe miili yetu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu." Yatulazimu kuilinda miili yetu. Miili ni hekalu la Mungu.

Akili zetu ni lazima zipewe Mungu kwa matumizi Yake. Twapaswa kuzijaza akili zetu na mawazo ya fikira zilizo nzuri. Yatulazimu tuzitumie katika kujifunza Neno la Mungu, kusudi lake, na njia Yake. Hayo yatatupa bidii kufanya yote anayotuambia kufanya.

Hivyo mali zetu zitapewa kwa kazi ya Mungu. Tutajazwa na Roho wake katika kujitia sisi wenyewe, upendo wetu, miili na akili zetu. Kutoa yote tuliyo nayo itafuata. Mungu anaomba sehemu moja ya kumi tu, lakini tutapenda kutoa sadaka nyingi zaidi ya hii.

**Mwisho:** (Kiongozi)

Ebu na tuufunge mpango wetu wa leo kwa kusimulia hadithi. Pengine itatusaidia kuufahamu uwakili wetu sisi wenyewe. Kulikuwako na kijiji kidogo karibu na kanisa la Kibatisti. Kila wiki daktari na mhubiri walikuwa wakienda katika kijiji hiki wakiwaambia wakaaji wa kijiji juu ya Kristo na kuwaponya ugonjwa wao. Wengi walikiri imani katika Kristo. Siku moja mjumbe wa kabila la kijiji hicho alikuja. Alipendezwa sana akawa mwenye furaha nyingi hata alitaka kuwa Mkristo pia. Kwa hiyo alirudi nyumbani mwake na kuchukua mali yake iliyokuwa nzuri sana. Aliutoa mkuki wake, mishale na miti yake, na vitu vinginevyo ambavyo vilikuwa vizuri sana. "Chukua hivi. Nataka kuwa Mkristo." Wamisheni walimweleza kwamba Mungu alitaka ajitoe nafsi yake kwanza naye ataokolewa. Bila ufahamu mjumbe alisema, "Ndivyo, ninayo akili na mimi ni kiongozi. Nitawakusanya watu wangu kila siku na kuwafundisha kutoka kwa kitabu chake Mungu. Halafu

Mungu, kwa hiyo walikata shauri kwamba kitu cha pekee ambacho wangefanya kilikuwa ni kujitoa wao wenyewe. Hii iliwabidi kufanya kazi masaa mengi zaidi.

Walifundisha madarasa kanisani, wakawasaidia akina mama wakati wa ibada kwa upande wa watoto wachanga, wakamsaidia mchungaji wao katika kazi yake. Siku moja walikata shauri kwamba watakuwa Wakristo wanaofanya kazi siku zote watakapokuwa wamemaliza masomo yao. Mchungaji alifurahi sana, lakini aliwaambia, "Mmekwisha kuwa wafanyi kazi wa siku zote, kwa sababu mmempa Mungu kitu muhimu, yaani nafsi zenu."

**Sehemu ya Pili:** Toa Upendo Wako

Upendo ni nini? Mungu ni pendo; na alikupenda wewe hata alimtoa Yesu ili wewe pamoja nami tutakuwa na maisha ya milele. Ulipomkiri Kristo upendo wake uliingia moyoni mwako. Upendo huu ulikuwa mnyofu, kama upendo wa mtoto mchanga kwa wazazi wake. Tunapogeuka kuwa Wakristo wenye nguvu, tunaanza kufahamu uweza wa upendo huo.

Samweli alikuwa na umri wa miaka 18 alipogeuka kuwa Mkristo. Kwa mara ya kwanza katika maisha yake yote, alijazwa na upendo, upendo wa Mungu. Alipozidi kukua katika ufahamu wa Mungu na Kristo, upendo wake uliongezeka vile vile. Alifanya kazi kwa bidii akishirikiana upendo wa Mungu na jamaa yake pamoja na marafiki. Katika huruma zake kwa wengine aliweza kutenda kazi nzuri sana kwa Mungu. Upendo ulimpa nguvu za kumwezesha kushuhudia katika jina la Kristo. Ingawa Samweli alikuwa mdhaifu, upendo wake ulimfanya kuwa mwenye nguvu.

**Sehemu ya Tatu:** Toa Yako Yote

Mkristo anapojitoa mwenyewe na upendo wake, atapenda kutoa yote aliyo nayo. Mungu hatuulizi kufanya zaidi kuliko





jinsi ya kuomba. Katika kuabudu kwetu katika ibada twaweza kuwaangalia viongozi wetu wa Kikristo wakati waombapo. Twaweza kufuata wakati waongozapo. Katika mikutano yetu ya Ushirika wa Wanawake, tunaweza kujifunza kuwa na sehemu katika ibada. Kwa kusoma sehemu ya mpango, huwa na tumaini kwamba Mungu atatusaidia katika yote tufanyapo. Hofu yetu ya kuzungumza kwa niaba ya Kristo na kuzifanya kazi za uongozi kanisani zitatoweka. *Kanisa letu ni mahali pa kujifunza Neno la Mungu. Ni mahali pa kujifunza jinsi ya kuomba na jinsi ya kujishughulisha kwa bidii katika kazi yake.*

**Sehemu ya Nne:**

Sababu nyingine muhimu ya kuhudhuria kanisani ni kwamba twaweza kuingia "mlangoni mwake kwa kushukuru, nyuani kwa kusifu." Wakati Kristo anapoendelea kuwa halisi katika maisha yetu, twazidi kuwa wenye shukrani kwa zawadi zake zote anazotupa. Twapaswa kwenda nyumbani mwake, kanisani, kumsifu Mungu kwa sauti zetu na mioyo yetu.

Je, wewe huenda kanisani ukiwa na kusudi moja la kusema "asante Mungu" kwa uzima wa milele na kwa ajili ya Yesu Kristo Mwanawe, kwa ajili ya mvua, jamaa, nyumba na kwa ajili ya upendo, n.k.? Mungu ni mwema. Yeye ni upendo. *Kanisa letu ni mahali pa sifa na shukrani.*

**Mwisho:** (Kiongozi)

Sasa, ebu tutaje sababu za kuhudhuria kanisani. (Ongoza kundi kwa kutoa majibu). Tunahudhuria kanisani ili kuabudu pamoja na ndugu na dada zetu katika Kristo. Tunaenenda kusikiliza Neno lake Mungu ili liweze kuwa sehemu ya maisha yetu. Tunajifunza njia nzuri ya kuwa Mkristo na kumtumikia Mungu. Mwishowe, twaenda kwenye nyumba ya Mungu kuimba sifa za jina Lake na kuonyesha shukrani zetu kuhusu pendo Lake. Kwa kufanya vitu hivi vyote tutatembea karibu na

Mungu na kwa uwezo wake atayatawala maisha yetu. Kwa kuufunga mpango wetu, ebu na tusome Zaburi 100 sote pamoja.

**Maombi:**

Mwe na wakati wa maombi ya moyoni ili kila mmoja ataweza kufanya upya nadhiri yake kwa Mungu kuishi kwa ajili Yake kila dakika ya kila siku na zaidi sana kuwa waaminifu katika mahudhurio ya kanisa.

Tuwaombee Wanawake Wabatisti wa Bara Kuu la Afrika wanapokutana Limuru. Tuombe ili pendo la Kikristo liweze kuutawala mkutano huo. Tuombe ili kazi ya Wanawake Wabatisti wa Afrika iweze kudumishwa.





Mpango wa Nne

## UWAKILI BINAFSI

**Maandiko Matakatifu:** Mithali 23:26

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Tena walitenda hivi si kama tulivyotumaini tu, bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu."*

*2 Wakorintho 8:5*

**Utangulizi:**

Kwa muda wa wiki tatu tumejifunza jinsi tuwezavyo kuwa Wakristo wazuri katika uaminifu wetu wa kuhudhuria kanisani, katika desturi nzuri za maombi, na katika kujifunza Neno la Mungu kila siku. Tunapofanya vitu hivi kwa kawaida tutataka kujitoa kabisa kwa Kristo. Ukristo unaofaa ni dini ya kujitoa. Mungu alimpa mwanadamu maisha. Alitupa sisi zawadi kubwa sana ya Mwanaye Yesu. Kwa kumfuata tumeombwa kutoa. Tunaweza kutoa nini?

**Sehemu ya Kwanza:** Toa Nafsi Yako

Hili ni jambo gumu kulitimiza. Mara nyingi ni rahisi kuvitoa vitu kuliko kujitoa nafsi yako. Katika 2 Wakorintho 12:14 twasoma "Sivitafuti vitu vyenu, bali nawatafuta ninyi." Kwa hiyo, kabla ya kuanza kuudhika na utoaji wa vitu tulivyo navyo mikononi mwetu, yatulazimu tupende kujitoa sisi wenyewe binafsi. Twaweza kufanya hivi tukikubali kubadilisha tamaa zetu na matakwa yetu kuwa yale ya Mungu.

Katika kijiji kimoja kulikuwa na wasichana wawili wa Kanisa la Kibatisti. Wote wawili walikuwa Wakristo wema. Hawakuwa na pesa zo zote. Kwa kweli, walikuwa na shida nyingi kwa kulipa karo zao za shule. Lakini walitaka kumtumikia

1. Soma Biblia kila siku.
2. Tafuta saa nzuri na mahali pa somo la kila siku.
3. Fuata mpango wa kusoma.
   a. Isome Biblia nzima moja kwa moja.
   b. Fuata taratibu ya kalenda ya kusoma Biblia kila siku.
   c. Jifunze Maandiko Matakatifu ambayo hutumiwa katika masomo ya Shule ya Jumapili.

Ikiwa utafuata madokezo haya, utapata misaada mingi katika funzo la Neno la Mungu. Vile vile, utagundua njia mpya za kujifunza na kukitumia kitabu chake, yaani Biblia.

**Maombi:**

Ebu na tuiombee kazi mpya ambayo imeanzishwa katika Tanzania kwa mpango wa "Bega Kwa Bega."





Mpango wa Pili

## MAOMBI

**Maandiko Matakatifu:** Mathayo 6:7-13

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla nyinyi hamjamwomba."*

*Mathayo 6:7-8*

**Kiongozi:**

Kabla hatujaona hitaji la maombi ni lazima tutamani ushirika wa haki kati yetu na Mungu. Yeye ni Baba yetu nasi tu watoto wake. Unamjuaje baba yako binafsi? Umepata kuzungumza naye? Kwa kweli twamjua kwa sababu tumeishi naye, tumezungumza naye, tumemsikiliza wakati atusaidiapo kukua kuanzia watoto wachanga mpaka kuwa watu wazima. Ulipokuwa mchanga ulifanya mazungumzo yote na baba yako? Hasha, ulisikiliza zaidi. Ulipokwenda kwake kwa msaada au ukiwa na tatizo, uliamini jibu lake?

Maombi ni kuzungumza na kutembea pamoja na Mungu, Baba yetu aliye mbinguni. Twahitaji kuenenda kwake kila siku katika maombi. Wakati tuombapo, twapokea uongozi katika kazi yetu ya kila siku. Si kuzungumza naye tu, lakini zaidi twahitaji kusikiliza kwa upole anapolidhihirisha kusudi Lake kwa maisha yetu. Leo tutajaribu kuyajibu maswali haya juu ya maombi. Kwa nini, wapi, jinsi gani na kwa ajili gani?

**Sehemu ya Kwanza:**

Katika Agano Jipya twasoma kutoka katika Mathayo 26 kifungu cha 41: "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho ni radhi, lakini mwili ni dhaifu." Kunazo sababu nyingi za kutufanya kuomba. Twapata nguvu kuyashinda majaribu yetu kwa kumwendea Baba yetu katika maombi. Katika kuomba bila kukoma Mungu anaweza kuzungumza nasi ili tutumike katika kazi zake.

Beslika alikuwa akizungumza na mchungaji wake. Walikuwa wakijadiliana juu ya maombi yake. Kwa muda wa majuma kadha alikuwa amefanya juhudi kubwa kutumia muda fulani kila siku katika maombi. Alikuwa na furaha kwa sababu alikuwa ameanza kuona jinsi lilivyokuwa jambo la ajabu kuzungumza na Mungu katika maombi. Haya ndiyo aliyoyasema. "Tangu nilipoanza kwenda kwake Mungu wangu katika maombi, nimekuwa na furaha kubwa. Siku zangu zimejaa na furaha na amani. Sasa ninazo nguvu za kuzishinda shida zangu na kuwa Mkristo mwema. Kabla sijaanza kuomba kila siku, mara nyingi nilisahau kutenda kama Mkristo. Lakini sasa maombi ni ya maana sana kwangu hata siwezi kuyasahau."

**Sehemu ya Pili:** Wakristo Humwomba Mungu Wakiwa Wapi?

Wakati upendo alipokuwa akifanya kazi shambani, moyo wake ulikuwa mzito. Yalikuwa majuma kadha tangu alipomzika mtoto wake wa kiume, lakini hata hivyo, angali akimkosa sana. Aliangalia angani iliyong'aa na kuomba hali akifanya kazi, "Mungu wangu, mimi ni mnyonge sana. Lakini wewe ni mwenye nguvu. Nisaidie katika wakati huu wa hitaji na upweke." Akiwa mle shambani, alijisikia mwenye nguvu mpya. Alikuwa Mkristo mwema na alikuwa amejifunza kwamba ataweza kumwomba Mungu mahali po pote.

Kulikuwa kungali na giza, Yohana alipoamka, ingawa kulikuwako na mwangaza mdogo upande wa mashariki. Kila





Yesu na kumsaidia kuwa Mkristo mwenye nguvu. Siku zingine, alisoma vifungu ambavyo alikuwa amesoma hapo mbeleni. Katika njia hii aliweza kujifunza Biblia yake kila siku.

**Sehemu ya Tatu:**

Beslika alikuwa mwenye kiti wa Ushirika wa Wanawake na Mkristo mwaminifu. Alizoea kuisoma Biblia yake kila siku kwa miaka kadha iliyopita. Jambo muhimu sana la kukumbuka juu ya mafunzo ya Biblia, alisema, ni kuweka saa fulani na mahali fulani kwa ajili ya kusoma na kujifunza.

Alipoanza kusoma Biblia kila siku kwa mara ya kwanza alikata shauri kuanza na kitabu cha Mwanzo na kuendelea kuisoma Biblia yote. Alifanya hivyo mara mbili kila mara akivumbua fikira mpya kumsaidia. Halafu alikata shauri tena kufuata kalenda kwa kusoma Biblia kila siku kwa mwaka mmoja. Alifanya hivi kwa uaminifu. Wakati mwingine alisoma Maandiko Matakatifu kila wiki ambayo yalihusiana na masomo ya Shule ya Jumapili.

Hivi majuzi alijifunza njia nyingine ya kujifunza Biblia yake. Mchungaji wake alikuwa akifundisha kitabu cha Yakobo. Mchungaji alimwuliza kila mmoja kusoma kitabu hiki kabla ya mwisho wa wiki. Kwa hiyo alijifunza kitabu kimoja kwa wiki nzima. Alifurahia, na ile wiki iliyofuata alianza kujifunza kitabu kingine. Mara nyingi alikuwa akijifunza moyoni vifungu maalum ambavyo vitamsaidia kumshuhudia Kristo vizuri.

**Mwisho:**

Basi, tutazame njia za kuwa wanafunzi wa Neno la Mungu. Tutaandika orodha ili ninyi nyote mwone. (Soma na kuandika juu ya ubao au karatasi kubwa, zungumzeni juu ya kila moja tena unapoisoma.)

Alipata majibu mawili kwa tatizo lake. Kwanza, alimwuliza mjukuu wake ambaye alisoma shuleni kufika nyumbani kwake kila siku na kumsomea. Wote wawili walitazamia wakati huu. Majuma yalipokuwa yakiendelea aliweza kulisikia Neno la Mungu kila siku, alianza kujazwa na Roho wake. Ushuhuda wake ulikuwa ushuhuda wa kila siku wa upendo wa Mungu. Pamoja na nafasi ya kulisikia Neno la Mungu mara nyingi, alijizoesha vifungu fulani ambavyo vilikuwa na maana maalum kwake. Alifanya kazi kwa bidii kwa kuviweka vifungu vingi moyoni mwake. Kwa hiyo mara nyingi alipotaka kusoma Biblia yake aliweza kuvisoma vifungu na kufikiria maana yake. Kwa upesi Biblia yake ilikuwa kichwani mwake na aliweza kuitumia wakati wo wote.

**Sehemu ya Pili:**

Sela Mwaponya alikuwa Mkristo mpya. Mumewe pamoja na jamaa yote hawakuwa Wakristo na ilikuwa vigumu kwake Sela kwenda kanisani mara nyingi. Lakini alienda kila mara alipokuwa na nafasi ya kufanya hivyo. Mchungaji wake alimwambia kwamba yeye kama Mkristo ni lazima alisome Neno la Mungu kila siku. Lakini hakuwa na Biblia na hakuwa na pesa za kununua moja. Angewezaje kulisoma Neno Lake kila siku ikiwa hakuwa na Biblia? Alipokwenda kwa mchungaji wake na kumwambia juu ya taabu zake, alimpa kitabu kidogo cha Yohana kutoka katika Agano Jipya. Alimwambia aanze kuziweka pesa zake ili aweze kuinunua Biblia.

Kila asubuhi baada ya mume wake kuondoka kwenda kazini, na watoto walikuwa wamekwenda shuleni, alikitoa kitabu chake kidogo cha Yohana na kuanza kukisoma. Aliweza kusoma vifungu vichache kila siku, mara nyingi akivirudia mara mbili au tatu. Wakati mwingine alifurahi sana na masomo hata hakuweza kuacha na aliendelea kusoma mlango moja au miwili. Alijaa na maneno ya ajabu ambayo yalimwambia juu ya





asubuhi alikata shauri kuamka mapema sana kabla ya jamaa na kutafuta mahali pasipo na kelele nje ya nyumba pa kukaa na kumwomba Mungu. Alijifunza Mathayo 6:8 ambapo huwaambia Wakristo kupata mahali pasipo na kelele ili waweze kuzungumza na Mungu. Aliona desturi hii kuwa yenye usaidizi mwingi. Kwa kufanya hivi kila siku, alipata nguvu mpya siku ile.

Twaweza kuomba tukiwa peke yetu, pamoja na wengine, kanisani, tukiwa kazini au nyumbani, lakini ni lazima tuwe na mpango wa maombi ili tuzungumze na Mungu ikiwa tunataka kukua kama Wakristo wenye nguvu.

**Sehemu ya Tatu:** Wakristo Huomba kwa Ajili Gani?

Elika alipoanza kuomba kwa mara ya kwanza aliustaajabia wokovu wake na upendo wa Mungu hata ikambidi kuomba sikuzote maombi ya shukrani. Aliona kwa mara ya kwanza vitu vyote ambavyo Mungu alikuwa amempa. Afya nzuri, mume mzuri na watoto, nyumba, mvua, udongo, jua ambalo lilisaidia mimea yake kukua. Kwa hivyo alimshukuru Mungu kwa hayo yote.

Kwa upesi alianza kufahamu ya kuwa hakuweza kumshukuru Mungu sikuzote na mara nyingi hakutenda kama Mkristo anavyopaswa kufanya. Kwa hiyo Elika alianza kumwomba Mungu katika maisha yake ya kila siku. Alimwomba amsamehe makosa mengi ya kila siku.

Kama alivyoendelea kujifunza zaidi juu ya Mungu na upendo wake, alikuwa na shauku ya kuwajulisha wengine habari za Mungu wake. Kwa hiyo alianza kuwaombea: baba yake ambaye hakuwa Mkristo, mumewe ambaye hakuwa na dini yo yote, watoto wake, kwamba watajifunza juu ya Yesu na kumwamini wakiwa wangali wadogo.

Haikumchukua muda mrefu kuona mahitaji ya marafiki zake na ya watu ambao hakuwajua hata kidogo. Kwa hiyo

aliomba kwa moyo mzito kwamba Mungu atawasaidia watu hawa na kumtumia yeye katika njia yo yote kueneza Neno Lake kwa wote.

**Sehemu ya Nne:** Wakristo Wanaombaje?

Mchungaji Edward alikuwa akilifundisha darasa juu ya maombi. Aliwaambia kuwa na moyo safi wanapoomba. Kwanza ni lazima kila mmoja aweke kando fikira zote kuhusu mambo ya dunia. Maombi yanapoendeshwa macho yanapaswa kufungwa na vichwa kuinamishwa. Wakati mwingine mtu anaweza kupiga magoti chini kabla ya kuzungumza na Mungu.

Katika Biblia tumeambiwa kuomba kwa njia ya imani na kuamini. Mara nyingi tunaomba Mungu kwa imani ndogo, na hata mara nyingi hatuna hakika kwamba maombi yetu yatajibiwa. Lakini tunapokua katika maisha yetu ya maombi imani yetu itaongezeka vile vile, na Mungu atatubariki pamoja na ushuhuda wetu wa Kikristo.

**Mwisho:**

Ebu sasa turudie baadhi ya njia ambazo maombi yanaweza kuwa yenye maana kamili katika maisha yetu. (Waulize wanawake kila swali, ukiwapa nafasi kujibu na kujadili, tena kutoa mawazo yao wenyewe. Hakikisha kwamba unajua majibu kabla ya wakati wa mkutano.)

Funga mpango huu kwa kusoma pamoja mfano wa maombi katika Mathayo 6:9-13. (Pengine waweza kufanya nakala nyingi za maombi haya kwa kumpa kila mwanamke aliyeko. Katika njia hii kila mwanamke ataweza kuichukua nakala yake nyumbani na kuitumia.)

**Maombi:**

Tuombe ili kuweze kuwa na Jengo la makanisa katika miji ya Migori, Mwingi, na Ng'arua, Kenya. Tuombe ili Wabatisti wa Kenya waweze kusaidia. Waombee wamisheni wa Jumuiya ya Kenya Timothy Musyoki, Andrea Kadamu, na Moses Nduthu.





Mpango wa Tatu

## MAFUNZO YA BIBLIA

**Maandiko Matakatifu:** 2 Timotheo 2:15

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."*

*2 Timotheo 2:15*


**Utangulizi:**

Kila Mkristo ambaye anataka kujifunza zaidi juu ya Neno la Mungu hana budi kukata shauri juu ya njia nzuri ya kujifunza Biblia yake kila siku. Kwa sababu tuna wajibu mbalimbali nyumbani na vile vile kwa sababu asili yetu ni mbalimbali, tutawaangalia wanawake kadha ambao wamepata njia zilizofaulu za kujifunza Neno la Mungu kila siku. Unapowasikia wanawake hawa; waweza kupata njia mpya ambayo itakusaidia. "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu" (2 Timotheo 2:15).

**Sehemu ya Kwanza:**

Mama Margaret alikuwa na watoto wengi na wote walikwenda shuleni kujifunza. Aliona fahari juu ya watoto wake, hasa kwa vile yeye hakujifunza kusoma wala kuandika. Katika Ushirika wa Wanawake alijifunza kwamba Wakristo wanapaswa kuisoma Biblia kila siku. Alipenda sana kwenda kanisani na kulisikiza Neno la Mungu likisomwa. Alisikiliza kwa makini sana ili aweze kukumbuka yote yaliyokuwa yakisemwa. Lakini aliwezaje kuisoma Biblia yake kila siku ikiwa hakuweza kusoma mwenyewe?

Ukichoka na kushona ua kubwa kwa viti vyote unaweza kushona ua hili dogo kwa viti vidogo yaani situli.







## MISAADA MAALUM

Nyumba yako itapendeza ikiwa utaipamba na vitambaa ulivyo fuma maua.

Chora maua haya kwenye vitambaa vya viti na meza. Tumia nyuzi rangi mbili ili vitambaa vionekane maridadi.





Ua hili unaweza kuchora kwa vitambaa vya kupamba nyumba yako. Inafaa hasa kwa viti.

Tumia uzi wa aina mbili tu. Ndiyo maua yatazidi kuonekana mazuri.

B

C